

LEKSIKOGRAFIA YA NADHARIA NA KISWAHILI

LEKSIKOGRAFIA YA KISWAHILA KAMA HAZINA YA KUPEVUSHA TAALUMA YA KISWAHILI

Nahashon Akungah Nyangeri

Chuo Kikuu cha Nairobi

nakungah@gmail.com

na

Enock Bitugi Matundura

Chuo Kikuu cha Chuka

mwagechure@gmail.com

Ikisiri

Lugha ya Kiswahili inadhihirisha utajiri mkubwa ambao haujafumbatiwa na wanaisimu kikamilifu. Utajiri wenyewe unadhihirika kutokana na wingi wa lahaja zake. Hii ina maana kwamba ikiwa kutaandikwa kamusi kamilifu ya Kiswahili, itakuwa kanzi kubwa na toshelezi, kinyume na kamusi zilizopo. Kwenye taaluma mbalimbali za isimu ya Kiswahili, leksikografia ni mojawapo ya taaluma zilizo changa katika isimu ya Kiswahili. Taaluma hii imedhihirisha kukumbwa na matatizo si haba yakiwemo uhaba wa wataalamu na machapisho, ingawa hii ndiyo taaluma ambayo inafaa kuwa imekoma mno kutokana na utajiri wa lugha hii. Hapa tunaona kwamba leksikografia ya Kiswahili imo kwenye njia panda. Hii ina maana kwamba pana haja kubwa ya wataalamu, watafiti na wapenzi wa Kiswahili kutafiti kwa kina kwenye uwanja huu kwa lengo la kupevusha taaluma hii. Makala hii inatalii matatizo na kutoa mapendekezo ya jinsi ya kuyatatua. Inazingatia haja ya kuzichunguza upya nadharia zinazotumika katika uandalizi wa kamusi. Nadharia za Leksikografia Amilifu pamoja na ile ya Vitendo Usemi zimetumiwa kudhihirisha jinsi ufanisi mkubwa unaweza kupatikana katika kuchimba maana kutoka kwa chimbo hili kwa ajili ya kutajirisha isimu ya Kiswahili. Hii ni pamoja na kuzingatia kueleza maana ya maneno kwenye kamusi. Mengine yatakayozingatiwa ni kubainisha udhaifu wa kushughulikia maana kwa mkabala wa kisemantiki katika kamusi huku mwegemeo wa mkabala wa kipragmatiki ukipewa kipaumbele. Hatimaye tumetoa mapendekezo kwamba ili kamusi iwe ya kufaa, inahitaji kuakisi muonoulimwengu wa jamii ya Kiswahili, kufafanua maneno kwa kuzingatia nadharia mseto za isimu, kuepuka maana zilizo changamano kwa kuzidadavua kwa usahili.